JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAJI**

**WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI**

Ofisi ya Meneja Ruwasa Wilaya
S.L.P 203,
**KARATU.**
Email:karatudm@ruwasa.go.tz

29.07.2024

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Karatu kwa niaba ya vyombo vya utoaji huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSOs) vya **JUWAMAKIHU, BAEWASU, ENDAWASU, BASHAWASU, GYEWASU, ENDAMIKO, MANG'OLA BARAZANI, LAGHANGARER** na **MALECKCHAND** anatangaza nafasi za kazi za wasimamizi (Fundi wakuu) na Afisa hesabu/ mtunza fedha wa vyombo vya utoaji huduma za maji ngazi ya jamii (CBWSOs) tajwa hapo juu kama ifuatavyo:-

1. **Fundi Mkuu/Msimamizi wa Mradi (Supervisor)- Nafasi 8**

**Sifa za mwombaji**

i. Awe mtanzania mwenye akili timamu na anyejua kusoma na kuandika.
ii. Awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi.
iii. Awe na cheti cha ufundi stadi Maji daraja la tatu (Trade Test Grade III/CBET Level I) au zaidi.
iv. Awe na uzoefu wa kufanya shughuli za ufundi katika miradi ya Maji kwa kipindi kisichopungua mwaka 1.
v. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi 45.
vi. Awe na uwezo wakutumia kompyuta (word, excel, internet, accounting software's etc.),
vii. Awe ni mtu muadilifu na mwaminifu na ambaye hajawahi kushtakiwa kwa tuhuma zozote.
viii. Awe na uwezo wa kufanya kazi pasipo kusimamiwa pamoja na uwezo wa kuwasimamia watumishi waliochini yake.
ix. Wasimamizi wa vyombo ya utoaji huduma ya maji ngazi ya jamii **MANG'OLA BARAZANI, GYEWASU NA ENDAWAU** wawe na cheti cha Diploma ya ufundi bomba kutoka chuo cha maji au chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

**Majukumu ya Fundi Mkuu/Msimamizi wa Mradi (Supervisor)**

i. Atafanya kazi chini ya kamati ya chombo (Community Water Committee).
ii. Atakuwa ndiye msimamizi na mtendaji mkuu wa shughuli za kila siku za chombo.
iii. Atakuwa ndiye katibu wa chombo na katibu wa vikao na mikutano yote ya chombo.
iv. Ataandaa na kusimamia utaratibu wa maandalizi ya vikao na mikutano yote ya chombo.

MENEJA WA RUWASA
KARATU

v. Atakuwa na jukumu la kusimamia utoaji wa huduma bora ya maji kwa wateja wote.
vi. Kusimamia matengenezo yote ya miundombinu ya maji na kuhakikisha kuwa huduma ya maji inapatikana kwa wakati.
vii. Kuandaa taarifa zote za usimamizi, uendeshaji na matengezo ya mradi wa maji za kila mwezi, kila baada ya miezi matatu, kila nusu mwaka na taarifa za mwaka na kuwasilisha katika kikao cha kamati ya maji ya chombo.
viii. Kuaandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya mradi na huduma ya maji na kusimamia mapato yote na matumizi ya chombo cha huduma ya maji.
ix. Kuhamasisha uchangiaji wa huduma ya maji na kutatua ama kutoa suluhisho la migogoro yote baina ya wateja na chombo.
x. Kusimamia manunuzi ya vifaa vya mradi na huduma ya maji kwa kufuata taratibu zote za manununzi.

**2. Afisa hesabu/ mtunza fedha- (msimamizi wa hesabu za chombo) – nafasi 5**

**Sifa za mwombaji**

i. Awe mtanzania mwenye akili timamu na anyejua kusoma na kuandika.
ii. Awe na elimu ya kuanzia kidato cha nne na kuendelea
iii. Awe na cheti cha uhasibu daraja la tatu au zaidi
iv. Awe na umri usiopungua miaka 18 hadi miaka 45
v. Awe na uwezo wakutumia kompyuta (word, excel, internet, accounting software's etc.),
vi. Awe ni mtu muaminifu na mwadilifu na ambaye hajawahi kupatikana na hatia ya kosa lolote

**Majukumu ya Afisa hesabu/ mtunza fedha**

i. Atafanya kazi chini ya Fundi Mkuu/Msimamizi wa Mradi (Supervisor).
ii. Atakuwa ndiye msimamizi wa mausuala yote ya fedha katika chombo
iii. Atasimamia na kupokea malipo ya maji na michango mbalimbali kwa kuzingatia taratibu zote za makushanyo ya fedha
iv. Ataandaa taarifa ya mapato na matumizi na kuiwasilisha kwa Fundi Mkuu/Msimamizi wa Mradi (Supervisor) kila mwezi, miezi mitatu, miezi sita na mwaka pamoja na kuziwasilisha katika vikao vya Chombo cha Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii na ofisi ya RUWASA Wilaya.
v. Kutunza vitabu vya fedha, hati za malipo mbalimbali na nyaraka zote za uthibitisho wa malipo mbalimbali/matumizi ya fedha ikiwa ni pamoja na kuandaa na kutunza kubukumbu/nyaraka zote za fedha
vi. Atafanya malipo baada ya kuidhinishwa na Fundi Mkuu/Msimamizi wa Mradi (Supervisor)
vii. Kushirikiana na Fundi Mkuu/Msimamizi wa Mradi (Supervisor) katika maandalizi ya bajeti ya mradi na kusimamia utekelezaji wa bajeti
viii. Pamoja na majukumu mengine atakayopangiwa na Chombo cha Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii na ofisi ya RUWASA Wilaya.

MENEJA WA RUWASA
KARATU

**MASHARTI YA KAZI NA MSHAHARA**

i. Ajira zote tajwa hapo juu ni za mkataba ya miaka mitatu (3) na miezi sita ya mwanzo itakua ni muda wa matazamio kabla ya kupewa mkataba.
ii. Mwombaji atakayefanikiwa kuajiriwa atalipwa mshahara kulingana na makusanyo pamoja na viwango vya mshahara viliyowekwa na Chombo cha Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii husika.
iii. Mwombaji awe tayari kufanya kazi katika eneo lolote atakalopangiwa na mwajiri wake.

**MAELEZO YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE**

I. Waombaji wote waandike barua za maombi kwa mkono.
II. Kwa wale waliosoma nje ya nchi ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU na NECTA) kulingana na ngazi ya cheti.
III. Maombi ya nafasi za kazi yawe na viambatisho vifuatavyo:-
    a) Wasifu binafsi (CV) yenye anuani za wadhamini wawili zikiwa na mawasiliano kamili (mdhamini awe na barua ya utambulisho kutoka kwa mtendaji wa mtaa/Kijiji anachokaa
    b) Nakala za vyeti mbalimbali vya taaluma (Kitado cha nne, sita, chuo cha ufundi, ujuzi, cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha Taifa/Namba ya NIDA) vilivyothibitishwa na mwanasheria/wakili.
    c) Picha ndogo (passport size) moja (1) iliyopigwa hivi karibuni.

Mwombaji mwenye sifa anatakiwa kutuma maombi kupitia posta au kupeleka ofisi ya RUWASA (W) Karatu kwa anuani ifuatayo;

**Meneja wa RUWASA (W),**
**S.L.P 203,**
**NMC-Karakana ya Halmashauri,**
**Karatu.**

Maombi ya kazi yanawezwa kutumwa kwa barua pepe karatudm@ruwasa.go.tz

Mwisho wa kupokea barua za maombi ni **tarehe 14/08/2024 saa 9:30 alasiri,** maombi yote yatakayowasilishwa baada ya muda huo **HAYATAPOKELEWA**.

***MUHIMU:***

1. Maombi ya wakazi wa maeneo ya miradi yatapewa kipaumbele,
2. Wanawake wanahamasishwa kuomba nafasi hizi.

**Tangazo hili limetolewa na;**

.............................................

Inj. Magai T. Kakuru
**Meneja wa RUWASA(W)**
**Karatu.**

MENEJA WA RUWASA
KARATU